THE
LUTHERAN
WORLD
FEDERATION

Department for Theology
Mission and Justice

lutheranworld.org

# TUNAMWAMINI ROHO MTAKATIFU: KARIBU KATIKA MAZUNGUMZO YA KIMATAIFA KUHUSU KUWA MLUTHERI

## Utangulizi

**Mchakato wa Utafiti wa Kimataifa Kuhusu Utambulisho wa Kilutheri: Tunamwamini Roho Mtakatifu:** Kati ya 2019-2022, FMKD linajishughulisha na utafiti wa kimataifa kuhusu utambulisho wa Kilutheri ulivyo sasa kama unavyojidhihirisha katika maisha ya kanisa katika muktadha wake wa sehemu husika. Mchakato wa utafiti unaonyesha nguvu ya tafakari ya kitheologia na unajenga fursa kwa ajili ya ushiriki wa watu wote. Lengo ni kusikiliza kwa njia ambazo zinatusaidia kuwa na sauti ya pamoja ya utambulizo wa Kilutheri kati ya utajiri wa utambulisho ulioko katika miktadha yetu inayovuka ushirika. Washiriki wa kongamano lililoandaliwa hapo awali walitengeneza maswali ya kuongoza mjadala wa kutafiti namna ubatizo, imani na desturi vinavyotengeneza namna Walutheri wanavyoyaishi mapokeo katika mazingira tofauti.

**Wewe ni wa muhimu katika mchakato huu!** Mazungumzo haya yapo wazi kwa ushirika mzima. Tunahimiza ushiriki mpana. Mwongozo huu wa mjadala ni nyenzo ya kusaidia mazungumzo katika ngazi ya kitaifa na ya eneo husika: makanisa ya kitaifa, dayosisi, majimbo, katika taasisi za kitheologia, miongoni mwa mabaraza ya sharika, mitaa, vikundi vya vijana, madarasa ya elimu ya Kikristo, au kwa ajili ya tafakari ya mtu binafsi.

Sharika au jumuiya zinazotekeleza hili zinahimizwa kuandaa tukio au mfululizo wa mazungumzo katika vikundi vidogo kujadili maswali haya. Mrejesho unaweza kuunganishwa katika fomu hii. Makundi yanaweza kuchagua kutafakari juu ya maswali yote, au wanaweza kuamua kulenga kwenye baadhi ya maswali kutoka kwenye kila kundi.

Majibu yanaweza kuandikwa kwenye visanduku vilivyowekwa. Sharika au vikundi vinaweza kutuma majibu yaliyounganishwa kwa makanisa yao ya kitaifa au mabaraza ya kikanda, au kurudisha kwa kutumia barua pepe hapo chini, zikionyesha wazi makanisa yao. Watu binafsi wanaweza kushiriki pia na kutuma majibu yao wenyewe. Majibu yaliyoandiwa yanaweza kutumwa kupitia barua pepe BeingLutheran@lutheranworld.org.

Njia mbadala ni kuwa washiriki wanaweza kutuma maelezo yenye ubunifu ambayo yamesukumwa na maswali haya. Tunakaribisha sanaa, muziki, au video kuonyesha kwa sanaa ya vitendo nini maana ya kuwa Mlutheri. Unaweza kutuma video, picha, sanaa, au nyaraka kupitia barua pepe BeingLutheran@lutheranworld.org.

**Majibu yako ni muhimu!** Majibu yatapokelewa hadi tarehe 1 Julai 2021. Habari zilizokusanywa ni njia mojawapo ya sisi kushiriki umoja na tofauti zetu kama ushirika. Utafiti ni wa siri, kwa maana kuwa majibu hayatatambuliwa yametoka kwa nani wakati wa kuchapisha matokeo. Tunaomba habari za utambulisho wako na eneo la kikanda

unalotoka ziandikwe vizuri. Uchambuzi utachapishwa na kutumwa kwa makanisa washirika na walioshiriki. Asante kwa kuchukua muda wako na kwa kushiriki.

## A. Habari za Mshiriki au Washiriki

1. **Wewe unatoka katika kanisa gani mshirika wa FMKD au katika taasisi ipi?**

| |
|---|
| |

2. **Wajibu wako ni upi katika kikundi (au nyajibu zinazowakilishwa na kikundi, kwa mfano, msharika wa kawaida, mwalimu, mwanafunzi, mchungaji, kijana, mdiakonia, n.k.)**

| |
|---|
| |

3. **Anwani ya kikundi au mtu binafsi:**

Jina: ____________________________________________________________

Barua pepe: ______________________________________________________

Jinsi: (Kiume/ Kike, au % ya uwiano wa Me/Ke) ___________________________

Umri (au kadirio la umri wa waliopo kwenye kikundi):

☐ chini 18

☐18-30

☐31-45

☐46-65

☐66 na zaidi

## B. Maelezo kwa ajili ya watu binafsi au kwa ajili ya kuongoza mazungumzo ya kikundi

Maswali yamegawanywa kati ya **Maswali ya Jumla** na **Maswali Maalumu ya Kikanda**.

***Maswali ya Jumla***: Maswali ya jumla ni kwa ajili ya washiriki, bila kujali maeneo yao. Kuna mafungu 5 ya maswali haya (*Utambulisho wa Kilutheri, Roho Mtakatifu kama Karama na Ahadi, Kanisa kama Ushirika, Tumebadilishwa na Kuwekwa Huru: Karama za Kiroho na Wito, Misheni na Kufanywa Upya*). Kila fungu lina maswali 6. Unaweza ukaamua kujibu kila swali, au kuchagua maswali machache kutoka kila fungu.

***Maswali ya Maalumu ya Kikanda***: Maswali yanayolenga maeneo yapo 5, ambayo yalitengenezwa kwa kushauriana na washiriki kutoka kila kanda za FMKD. Tafadhali jibu maswali ambayo yanahusiana na kanda yao.

Kila sehemu ina maelezo mafupi kuhusu mada na mstari wa Biblia unaohusiana na mada. Maswali ni ya wazi, yakikusudiwa kusaidia mjadala katika kikundi. Unaweza ukaandika majibu kama orodha ya mawazo makuu, kama muhitasari wa maelezo ya mazungumzo, au nukuu fupi. Visanduku vya kuandika majibu vimewekwa.

*Maelezo maalumu kwa ajili ya kusaidia vikundi*: Kama kanisa lako, kikundi katika usharika, darasa au taasisi vinaandaa mazungumzo ya pamoja, mtahitaji kuangalia juu ya namna nzuri ya kuongoza.

- Tengeneza mazingira ya ukaribisho na ukarimu.
- Weka wazi kiasi cha muda kitakachotumika kujadili kila swali.
- Anza na sala, mkimuomba Roho afungue mioyo yenu, aamushe mjadala wa kiimani, na mtumie fursa hii kulea imani ya ubatizo wetu, na umoja wetu katika mwili wa Kristo.
- Hakikisha kuwa mazingira ni salama kwa ajili ya kushirikishana, na kwamba kila mmoja ana nafasi ya kuchangia
- Mwishoni mwa kipindi, jipongeze ninyi kwa ninyi kwa kushiriki.

## C. Maswali ya Jumla

### *I. Kuhusu utambulisho wa Kilutheri (maswali 6)*

Utambulisho wetu wa kidini unaundwa ndani ya mifumo ya shughuli za kawaida na uzoefu ambao unahusisha mambo yote yanayokamilisha utambulisho, yaani *solae* (Neno tu, Neema tu, Kristo tu, Imani tu), mapokeo ya kiimani na kitheologia, mapokeo ya kiliturgia na kijamii ya watu wenye imani tofauti ambamo mapokeo yetu ya kitamaduni yanaundwa, kuwepo dini nyingi, na mifumo ya imani za kijadi au kienyeji. Kwa njia hii, Mapokeo ya Kilutheri yanaishi kila wakati, na misemo huafikiwa na kufanywa upya kila wakati.

- Taja madokezo ya awali 5 yanayoeleza nini maana ya kuwa Mlutheri?

- Utambulisho wangu wa Kilutheri ulijengwa na .... (*andika jinsi unavyofikiri*)

- Ni mapokeo gani unayaenzi katika kutekeleza imani yako?

- Ni mafundisho gani tofauti ya urithi wako wa Kilutheri yanaathiri maisha yako ya kila siku?

- Katika muktadha wako, ni mchango gani unatokana na:
  - ibada na muziki katika kujenga utambulisho wa Kilutheri?

  - Katekisimo ya Luther katika kujenga utambulisho wa Kilutheri?

  - Maungamo ya Kilutheri katika kujenga utambulisho wa Kilutheri?

- sala na matendo ya kiroho katika kujenga utambulisho wa Kilutheri?

- mapokeo ya kitamaduni, kikabila au waliokufa katika kujenga utambulisho wa Kilutheri?

- Ni tofauti gani ipo kwa wewe kuwa Mlutheri?

## II. *Roho Mtakatifu kama Karama na Ahadi (maswali 6)*

Maswali haya yanalenga juu ya Roho Mtakatifu. Katika Katekisimo Ndogo ya Luther, ukiri wa imani unatukumbusha kuwa imani yetu imejengwa ndani ya kazi za Utatu Mtakatifu. Katika Kristo, tunapokea Roho Mtakatifu kama zawadi na ahadi. Roho wa Mungu anaiumba na kuifanya upya dunia, anatuita na kutumiliki sisi kwa njia ya ubatizo ili tumzalie matunda ya kazi njema ndani yetu. Uumbaji ni uwanja kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Mungu anafanya kazi ndani ya dunia nzima.

Mstari wa Biblia: *Yohana 14:25- 27 "Nimewaambieni mambo haya nikiwa bado pamoja nanyi, lakini Msaidizi, Roho Mtakatifu,ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisheni kila kitu na kuwakumbusheni yote niliyowaambieni."Nawaachieni amani; nawapeni amani yangu. Siwapi nyinyi kama vile ulimwengu ufanyavyo. Msiwe na wasiwasi, wala msifadhaike."*

- Ni kwa njia gani unaona uwepo wa Mungu katika liturgia ya kanisa lako?

- Lini na wapi Roho Mtakatifu hufanya kazi?

- Ni kwa namna gani imani za kienyeji au za kijadi na mila za kitamaduni zinatambulisha wazo lako kuhusu Roho wa Mungu?

- Ni fursa zipi zipo kwa watoto na vijana katika muktadha wako kuchunguza au kulea imani?

- Ni njia zipi zenye nguvu sana hutumika na kanisa lako kueleza upendo wa Mungu katika muktadha wako?

## III. Kanisa kama Ushirika (maswali 6)

*Katekisimo inatufundisha kuwa kanisa ni sehemu ya ushirika wa watakatifu, ambamo Roho hutenda ili kututakasa na kutuumba. Ibada, muziki, na matendo ya kiroho yanayozungukwa na Neno na sakaramenti vinalea imani yetu, sambamba na alama zote za kanisa: sala, ushirika, mshikamano wakati wa mateso, huduma, mafunzo ya pamoja ya Biblia, na mengine mengi.*

Mstari wa Biblia: *1 Wakorintho 12:1-14 "Ndugu, kuhusu vipaji vya kiroho, napenda mfahamu vizuri mambo haya…Maana sisi, tukiwa Wayahudi au watu wa mataifa mengine, watumwa au watu huru, sote tumebatizwa kwa Roho mmoja katika mwili huo mmoja; na sote tukanyweshwa Roho huyo mmoja. Mwili hauna kiungo kimoja tu, bali una viungo vingi."*

- Unaweza ukaielezea vipi hali ya kiroho katika kanisa au muktadha wako?

- Ni jinsi gani nyimbo, maombi, na liturgia vinaongeza uelewa wako wa Roho Mtakatifu?

- Taja njia tatu ambazo unaona Roho Mtakatifu yupo kazini katika usharika au jumuiya yako?

- Ni kwa namna gani
    - sala inaathiri maisha yako ya kila siku?
    - Masomo ya Biblia yanaathiri maisha yako ya kila siku?
    - Ushirika Mtakatifu unaathiri maisha yako ya kila siku?

- Nini mchango wa vijana na watoto katika maisha ya kanisa lako au jumuiya unakoshiriki?

- Unafundisha namna gani mapokeo ya Kilutheri?

## IV. Nimebadilishwa na Kuwekwa Huru: Karama za kiroho na wito (maswali 6)

Maswali haya yanalenga juu ya mambo ya hali ya kiroho, na yanatualika kuchunguza uhusiano kati ya karama za kiroho na huduma. Roho Mtakatifu anazaa matunda kwa kila mmoja wetu. Kama sehemu ya ukuhani wa watu wote waliobatizwa, tunaitwa na tumewekwa huru kuelezea karama za kiroho (*charismata*) kwa njia ya huduma mbalimbali

katika dunia. Tunazipima karama za kiroho (*na hasa ukweli kuhusu aina tofauti za kiroho kama tunazopitia sasa)* kwa kutumia wito wa kibiblia kwamba karama wakati wote zinatumika kuujenga mwili wa Kristo kuelekea upatanisho na kupenda huduma kwa ajili ya jirani zetu.

Mstari wa Biblia: *Wagalatia 5:1, 22-25 "Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Basi, simameni imara wala msikubali tena kuwa chini ya nira ya utumwa… Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi…Tukiishi kwa msaada wa Roho, na tuufuate mwongozo wake.."*

- Ni kwa jinsi gani ubatizo wako unaathiri namna unavyoishi maisha yako ya kila siku
    - katika familia yako?
    - katika jumuiya yako?
    - katika kazi au eneo lako unalolipenda?
    - kama raia?
- Nini maana ya karama ya kiroho?
- Taja mpaka karama 4 za kiroho ambazo unazo?
- Ni kwa jinsi gani jinsia inaathiri namna kanisa linavyozungumzia kuhusu karama za kiroho?
- Ni kwa jinsi gani unaweza kuelezea karama zako za kiroho ndani ya kanisa lako?
- Ni kwa namna gani wewe au jamii yako inatambua tofauti kati ya karama za Roho na mapenzi ya mtu binafsi?

### *V. Misheni na Kufanywa Upya (maswali 6)*

Roho Mtakatifu anatuita na kutuandaa ili tushiriki katika Misheni ya Mungu. Walutheri wanaendelea, kwa njia ya maombi na ushirikiano kurejea kwenye Biblia na kwenye mapokeo yetu ya kitheologia na kimaungamo wakiuliza maswali mapya ambayo yanajitokeza kutokana na uzoefu wao katika maisha. "Mzunguko huu wa kufasiri" ili kutambua wito wetu katika nyakati na muktadha wetu unatusaidia kupata maelezo mapya yenye ubunifu ya imani yetu inayoishi ambayo inazungumza na mambo ya sasa, hasa kuhusiana na ustawi wa jirani zetu, haki, utunzaji wa uumbaji, na uchumi wa maisha endelevu, upatanisho na kufanywa au kuamshwa upya kwa kanisa.

Mstari wa Biblia: *Zaburi 104: 30-31, "Ukiwapulizia pumzi yako, wanaishi tena; wewe waipa dunia sura mpya. Utukufu wa Mwenyezi-Mungu udumu milele; Mwenyezi-Mungu apendezwe na matendo yake mwenyewe."*

- Katika muktadha wako, ipi ni sehemu muhimu sana ya kazi ya Mungu katika dunia ya leo?

- Roho Mtakatifu anakuandaa namna gani katika kujishughulisha na:
  - masuala ya kijamii au ya kisiasa katika muktadha wako?
  - masuala ya kiuchumi katika muktadha wako?
  - kutunza uumbaji katika muktadha wako?
  - haki za kijinsia katika muktadha wako?

- Unaieleza vipi imani yako katika mazingira ya umma na dini nyingi?

- Je unaona Roho wa Mungu yupo kazini nje ya kanisa? Kama ndivyo kwa njia zipi?

- Je kanisa lako linakuza ustawi au uponyaji ili kuondoa kiwewe? Kama ndivyo, ni kwa njia gani?

- Ni wapi unaona dalili za kufanywa upya katika kanisa lako sasa? Ni wapi kanisa lako linahitaji kufanywa upya au kuwa na mabadiliko?

## D. Maswali Maalumu ya Kikanda

Tafadhali jibu masuali yanayohusiana na kanda yako ya FMKD.

### *Afrika (maswali 5)*

- Ni imani zipi za kienyeji, kijadi au za asili ambazo zinaunda mafundisho ya Kilutheri kuhusu Roho Mtakatifu?

- Unawajibu vipi watu wanaotumia vibaya karama za kiroho ili kupata faida za kifedha?

- Utambuzi wetu wa Kilutheri unatuandaa vipi kujibu mawazo kuwa Mungu anawabariki na vitu vya utajiri na mamlaka wanaoamini?

- Ni karama zipi mazingira yako yanachangia kwa mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Nini ambacho kanisa lako linahitaji kupokea kama karama kutoka kwa ushirika wa Kilutheri wa kimataifa?

### *Asia (maswali 5)*

- Ni kwa jinsi gani unamuona Roho Mtakatifu kati muktadha wa utamaduni wenu wa Kiasia?

- Ni kwa namna gani dini nyingi zinatambulisha uelewa wenu wa Roho wa Mungu?

- Ni kwa namna gani tunatatua mahitaji ya kiroho katika muktadha wetu

- Ni karama zipi mazingira yenu yanachangia kwa ajili ya mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Kanisa lako linahitaji nini kupokea kutoka kwa ushirika wa Kilutheri wa kimataifa?

*Ulaya ya Kati na Mashariki (maswali 5)*

- Ni kwa namna gani tunafafanua vizuri zaidi juu ya uhusiano wa karama za Roho na uelewa wetu wa kanisa?

- Je kimsingi Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa njia ya watu binafsi au katika jumuiya?

- Tunaelezaje wajibu wa Roho Mtakatifu kuwa Mfariji katika makanisa yetu? Je tunahitaji taasisi zaidi kwa ajili ya utunzaji kiroho, vituo vya kupumzikia, n.k., katika makanisa yetu?

- Ni karama zipi mazingira yako yanachangia kwa ajili ya mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Nini kanisa lako linahitaji kupokea kama karama kutoka ushirika wa Kilutheri duniani?

*Ulaya ya Kati na Magharibi (maswali 5)*

- Tunahusiana vipi na mihimili ya kijamii na kisiasa kama milki ya kazi ya Mungu?

- Ni changamoto zipi unakutana nazo katika kuieleza imani katika muktadha wako?

- Ni kwa jinsi gani unawafanya watu leo kuwa wanafunzi?

- Ni karama zipi mazingira yako yanachangia kwa mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Kanisa lako linahitaji nini kupokea kama karama kutoka ushirika wa Kilutheri duniani?

*Amerika ya Kusini na Visiwa vya Karibi (maswali 5)*

- Ni mapokeo gani ya asili kutoka historia yako yanaelezea Utambulisho wako wa Kilutheri?

- Ni kwa namna gani nyimbo za asili na matendo ya kiroho vinajenga ibada yako?

- Tunawezaje kutambua uwepo wa Roho Mtakatifu katika usharika?

- Ni karama gani mazingira yako yanachangia kwa mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Kanisa lako linahitaji kupokea nini kama karama kutoka ushirika wa Kilutheri duniani?

*Nodiki (maswali 5)*

- Je ubarikio wa wanawake na wanaume unawezaje kuwa kielelezo cha karama za Roho?

- Ni jinsi gani hali ya kuwa kanisa la watu inaelezea utambulisho wa Kilutheri wa kanisa?

- Ni kwa namna gani historia ya makanisa ya kiserikali na makabila yake yanaathiri namna tunavyozungumza kuhusu Roho?

- Ni karama gani mazingira yako yanachangia kwa mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Kanisa lako linahitaji nini kupokea kama karama kutoka ushirika wa Kilutheri duniani?

***Amerika ya Kaskazini (maswali 5)***

- Unatumaini vipi kuwa Roho Mtakatifu anaweza kujenga baadaye yako?

- Je unaona utambulisho wako wa Kilutheri unakuandaa kujibu changamoto za dunia?

- Unaamini ni wapi Mungu anatuita sisi kama kanisa?

- Ni karama zipi mazingira yako yanaweza kuchangia kwa mapokeo ya Kilutheri kimataifa?

- Kanisa lako linahitaji nini kupokea kama karama kutoka ushirika wa Kilutheri duniani?

## E. Maoni ya Jumla

**Je kuna jambo lingine zaidi ambalo ungependa kutushirikisha?**

## Asante kwa majibu yako! Ni mategemeo yetu kuwa tutaendelea kuwasiliana na wewe.